

Ilikuwa saa tatu asubuhi. Mbingu zilikuwa rangi ya samawati na hali ya hewa ilikuwa shwari. Ilikuwa ni siku ya furaha lakini wanyama wa pori walikuwa hawana furaha.

Sungura alikuwa chini ya mti. Alikuwa akisukasuka kichwa chake. "Sitaki kwenda! Siendi!" sungura alitamka. "Sitaki na sitokwenda!" alisema tena kwa ukali.

Karibu yake alikuwepo bweha akimnasihi sungura.

"Eh, bwana nenda. Tafadhali nenda. Mimi nakuomba uende."

Kila bweha akinasihi, sungura alizidi kutikisa kichwa chake na kusema, "Sitaki, wala siendi!"

Pambizoni kwenye kichaka kulikuwa na wanyama wengine wakichungulia. Nyati, twiga, paa, dikidiki, ngiri, nungu na mbuni



walikuwepo. Wanyama wote walikuwa na wasiwasi. Pale porini palikuwa na simbamarara mmoja mkubwa na mwenye nguvu sana. Wanyama wote porini walikuwa wakimwogopa. Kila siku alikuwa akiwinda na kukamata wanyama.

Alikuwa akiwaua wanyama watatu au wanne lakini alikuwa hali zaidi ya mnyama mmoja. Alikuwa akiwaua wanyama wengi zaidi ya mahitaji yake. Wanyama wa porini walikuwa na hofu kubwa juu ya simbamarara. Walikuwa hawana furaha.

Siku moja bweha alifikiria jambo la kufanya. Aliwaita wanyama kwenye mkutano.

Baada ya kuzungumza kwa muda mfupi, bweha alikata shauri akasema, "Tukubaliane kuwa mmoja kati yetu apelekwe kwa simbamarara kila siku awe ni chakula chake. Waliobaki siku hiyo hawatakuwa na wasiwasi kwa sababu simbamarara hatatafuta chakula siku hiyo."

Wanyama wote walikubali rai hii ya bweha. Simbamarara pia alikubali. Simbamarara alipenda rai ya kupelekewa chakula pangoni pake pasi na yeye kujisumbua kwa kuwinda lakini bweha alikuwa mjanja. Aliwaza hivi moyoni mwake, 'Nitawapeleka kwanza wanyama wadogo wadogo na wale ambao hula majani. Zamu yangu itakuwa mwisho kabisa.'

Sasa twafahamu kwa nini wanyama walikuwa na wasiwasi. Walijua kuwa chakula cha simbamarara kikichelewa, atatoka mwenyewe kuwawinda kama hapo mbeleni. Lakini hakuna mnyama ambaye aliweza kumlazimisha sungura kwenda. Hakuna vile vile mnyama aliyetaka kujitolea na kwenda badala ya sungura. Wanyama walimlaumu sungura kwa



kuvunja mkataba wao na simbamarara.

Lakini sungura aliwajibu, "Msinisumbueni. Mimi nina mpango wangu wa kuwaokoa nyote msiliwe."

Msamiati

shwari	:	hakuna upepo.
sukasuka	:	tikisa; chezesa.
nasihi	:	shauri kwa kutoa maneno matamu.
pambizoni	:	kandokando.
mahitaji	:	haja.
kujitolea	:	kufanya jambo bila kulazimishwa.
mkataba	:	masikizano.
sumbua	:	tia tabu.
okoa	:	ondosha katika hatari.

A. Ufahamu

1. Jibu maswali haya:

- Bweha alitaka sungura aende kwa nani?
- Ni ndege gani aliyetajwa katika hadithi hii?
- Mahitaji ya chakula cha simbamarara kila siku yalikuwa ni wanyama wangapi?
- Kwa nini wanyama walimlaumu sungura?
- Je, wanyama waliweza kumlazimisha sungura kwenda?
- Bweha alikuwa na mpango wa kuwapeleka wanyama wa aina gani kwanza kwa simbamarara?